

# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM



## CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU MKWAWA

### ***KUFUNGWA KWA CHUO***

Wanafunzi, wanataaluma na Jumuiya ya Mkwawa mtakumbuka kwamba baada ya kumaliza mitihani ya mwisho ya muhula wa kwanza wa mwaka wa masomo 2019/2020, Chuo kilifungwa kwa muda wa wiki tatu, kuanzia tarehe 29 Februari mpaka 22 Machi 2020. Kutokana na taarifa zilizotolewa na Serikali kwamba Tanzania kwa sasa inakabiliwa na ugonjwa wa CORONA (COVID-19), Chuo hakitafunguliwa tarehe 22 Machi 2020. Kufungwa kwa Chuo kunafatia hatua madhubuti za Serikali za kuepusha kuenea kwa ugonjwa huu. Tarehe ya kufungua Chuo itatangazwa mara tutakapopata mwongozo.

Aidha, wanafunzi wote, katika Vitivo vyote, ambao kwa sababu mbalimbali bado wapo Chuoni wanatakiwa kuwa wameondoka ifikapo Ijumaa tarehe 20 Machi 2020, hadi hapo watakapotaarifiwa kurudi tena Chuoni.

Shughuli nyingine zote za Chuo zitaendelea kama kawaida. Watumishi wote wanakumbushwa kuzingatia maelekezo kuhusu namna ya kujikinga na kumkinga mtu mwingine na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona.

**IMETOLEWA NA  
PROFESA ESTHER W. DUNGUMARO  
RASI WA CHUO**

**19 Machi 2020**